



TOLEO NA.04

Tovuti: www.nsimbodc.go.tz

Nsimbo Wiki hii

Tunatekeleza



FEBRUARI 23, 2019

Watendaji Kata ,Vijiji Nsimbo wanolewa

- ⇒ *Wakumbushwa jukumu la usimamizi wa Ardhi kuondoa Migogoro,*
- ⇒ *Wasisitizwa kutumia Sheria ndogo kuleta nidhamu ,Uwajibikaji kwa Wananchi,*
- ⇒ *Wananchi Wasiohudhuria vikao bila sababu Mwarobaini waandaliwa .*

Habari zaidi Uk.....2



Pichani:Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali watu Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Betuely Ruhega akizungumza wakati wa Kikao kazi cha Watendaji wa Vijiji na Kata kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Februari 21,2019.(Picha na Mpiga Picha wetu)

Watendaji Kata, Vijiji Nsimbo wanolewa.....

Na **John Mganga,**

Nsimbo –Makao Makuu

Watendaji wa Kata na Vijiji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wametakiwa kusimamia kikamilifu Sheria ndogo za Halmashauri ili kuhakikisha kuwa nidhamu na uwajibikaji kwa Wananchi vinakuwepo ili kuharaki-sha maendeleo.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Raphel Kalinga** Februari 19, 2019 akifungua kikao kazi cha Watendaji wa Vijiji na Kata kilichoandaliwa na Idara ya Utawala na Rasilimali watu kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

Akizungumza na Watendaji hao, Mwenyekiti Kalinga amesema kitendo cha baadhi ya Wananchi Nsimbo kutohudhuria vikao mbalimbali vinavyoandaliwa katika ngazi ya Vijiji na Kata imekuwa sababu mojawapo ya Wananchi hao wakaidi kuwa na uelewa mdogo kuhusu masuala mbalimbali ya Kiserikali hali inayopelekea ushiriki mdogo katika uchangiaji nguvu kazi katika Miradi mbalimbali ya maendeleo hali inayozorotesha maendeleo.

Kutokana na kukithiri kwa tabia hiyo **Mh.Kalinga** amewataka Watendaji hao wa Kata na Vijiji kuhakikisha kuwa wanatumia kikamilifu Sheria ndogo ikibidi kutozwa faini wote wanaobainika kutohudhuria Vikao pasipo na sababu za msingi.

Aidha **Mwenyekiti Kalinga** amewakumbusha Watendaji hao jukumu kubwa la usimamizi wa ardhi ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika kutatua Migogoro mbalimbali ya ardhi katika maeneo yao kwa kuwa wao ndio wanaishi na Wananchi hao.

Amesema Viongozi wa ngazi za juu Wanawategemea zaidi Watendaji wa Vijiji na Kata katika kutekeleza majukumu mbalimbali likiwemo la usimamizi na utatuzi wa Migogoro mbalimbali ya ardhi kwa kuwa wao ndio wanaoishi na wanaofahamu kwa sehemu kuwa Maeneo na Jamii wanayoishi nayo.

Amesisitiza juu ya muhimu wa Watendaji wa Kata na Vijiji kuwa makini na wawekezaji wanaofika katika maeneo yao kwa lengo la kuhodhi ardhi kuhakikisha kuwa watu hao wanafuata sheria kanuni na taratibu ili kuepusha Migogoro ya ardhi

Awali Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali watu **Bw.Betuely Ruhaga** akimkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri ameeleza kuwa Kikao kazi hicho kinafanyika ikiwa ni sehemu ya utekelezaji Majukumu ya Idara ya Utawala kuwakumbusha watendaji hao majukumu yao ya kila siku kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa utoaji huduma kwa Wananchi ambapo mada kadhaa ziliwasilishwa na Maafisa Utumishi mbalimbali wa Idara hiyo.



Pichani:Sehemu ya Watendaji wa Vijiji na Kata Nsimbo wakati kikao kazi cha kuwajengea uwezo kikiendelea. Katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri (Pcha na John Mganga.)

Mabaraza ya Kata kujengewa uwezo Nsimbo.....



Pichani:Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria Nsimbo Bw.Nelson Hutty akiwasilisha mada katika Mafunzo ya kujenga uwezo kwa Mabaraza ya Kata za Nsimbo Mtapenda na Kapalala Februari 21,2019

Na John Mganga,

Nsimbo –Makao Makuu

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia Kitengo cha Sheria Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeanza kutoa elimu kwa mabaraza ya Kata yanayohusika katika kujadili mashauri mbalimbali ya utoaji Haki katika ngazi za Vijiji na Kata.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria Nsimbo **Bw.Nelson Hutty** amesema lengo la kutoa Elimu ya Masuala mbalimbali ya Sheria kwa Mabaraza hayo ya Kata ni kuyajengea uwezo mabaraza

hayo uelewa wa Sheria mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mabaraza hayo yanazingatia Sheria katika kujadili mashauri mbalimbali ili yaweze kutoa haki na kuondoa kabisa migogoro katika Jamii

Bw.Hutty amesema Migogoro mingi katika Jamii ikiwemo ya ardhi imekuwa ikiendelea kukua na kushamiri katika maeneo mbalimbali Nchini kutokana na Mabaraza ya Kata kutokuwa na Uelewa wa kutosha wa Sheria mbalimbali za Nchi kwa mabaraza ya Kata hali inayopelekea kukiuka sheria katika utoaji haki katika mashauri mbalimbali.

Kutokana na changamoto hiyo **Bw.Hutty** amesema ku-

jenga uelewa wa Sheria mbalimbali mara kwa mara kwa mabaraza ya Kata kutaihakikishia Jamii uhakika wa upatikanaji haki katika Mashauri mbalimbali kutokana na mabaraza hayo kuwa na uelewa kuhusu Sheria mbalimbali na mabadiliko yake ya mara kwa mara.

Ameeleza kuwa uelewa mdogo wa Sheria mbalimbali kumekuwa sababu kubwa ya ukiukwaji wa haki katika utoaji maamuzi katika mashauri mbalimbali ya Kijamii

Katika kutekeleza hilo Kitengo cha Sheria Nsimbo Februari 21, 2019 kimeanza kutoa Elimu ya Sheria kwa mabaraza ya Kata ikihusisha mabaraza ya Kata za Kapalala na Mtapenda na Nsimbo ambapo Kitengo hicho kimejipanga kuzifikia Kata zote kuanzia Februari 24 na kuendelea.

Mada zinazowasilishwa katika Mafunzo hayo kwa mabaraza ya Kata ni pamoja na Sheria ya Ndoa, Sheria ya Ardhi, ambapo mbali na Kaimu mkuu wa Kitengo hicho Bw.Nelson Hutty ,Wanasheria wengine watakaowasilisha mada ni Mugea Masambu, pamoja na Wakili Josephine Chilongozi wote wa Kitengo cha Sheria Nsimbo.

Mwenge wa Uhuru kutua Nsimbo Aprili,2019



Pichani : Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi Meja Jenerali Mstaafu Raphael Muhuga (Kulia aliyevaa Kapelo Nyeupe) alipokabidhiwa Mwenge wa Uhuru na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mh.Agrey Mwanri May 2,2018 katika Uwanja wa Ndege Mpanda. Kabla ya kukimbizwa Katika Halmashauri za Mkoa wa Katavi (Picha na Maktaba Nsimbo HQ)

Na John Mganga-NDC

Nsimbo- Makao makuu

Mwenge wa Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatarajia kuwasili Nsimbo Aprili 13, 2019, mratibu wa Mwenge Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Alex Wema Magessa amedokeza.

Magessa ameeleza kuwa taarifa za kuwasili kwa Mwenge wa Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Nsimbo ni kwa mujibu wa ratiba ya Shughuli za Mwenge iliyotolewa na Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge,Kazi Vija-na,Ajira na Wenye ulemavu.

Mratibu wa Mwenge Nsimbo ameeleza kuwa Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu 2019 yatakua ya aina yake kutokana na namna ambavyo Ofisi yake imelipa uzito wa kipekee suala hilo.

Amesema kuwa kwa sasa Nsimbo inaandaa miradi itakayozinduliwa na Mwenge na kwamba Ofisi yake itaendelea kuwajua Wananchi hatua mbalimbali za maandalizi ya Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru.

Aidha ameongeza kuwa Miradi itayozinduliwa Nsimbo kwa mwaka huu ni miradi ya Kihistoria kwa kuwa inalenga kui-

marisha zaidi utoaji huduma kwa Wananchi.

Kwa mwaka 2018 mwenge wa Uhuru uliwasili Nsimbo na kupokelewa katika Kijiji cha Mtapenda Kata ya Mtapenda Aprili 4, 2018 na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo ulikabidhiwa katika uwanja wa Mpira wa Kanoge kabla ya kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbe-we.

TANGAZO

Februari 23,2019

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inawatangazia Wananchi wote wanaohitaji kununua Mbegu za Korosho kuwa ,

Kwa sasa,

Mbegu za Korosho zinapatikana Katika Ofisi za

Watendaji wa Kata za Kapalala,Mtapenda na

Itenka

Hivyo wale wote wanaohitaji Mbegu hizo wawasiliane ama wafike katika Ofisi tajwa kwa maelekezo zaidi.

Tangazo hili limetolewa na;
Idara ya Kilimo na Ushirika
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

Jarida hili la Wiki Nsimbo huandaliwa na kutolewa na
Kitengo cha Teknolojia ya Habari Mawasiliano na
Uhusiano Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ,Halmashauri
ya Wilaya ya Nsimbo,Ofisi Na.2

Mawasiliano:

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

SLP 688,Mpanda Katavi

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz

Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

Tel +25546310716